East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 2, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 2, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mofolojia Isoshikanisho katika Kiswahili

*Deo Ngonyani*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Jimbo la Michigan, 619 Red Cedar Rd, B331 Wells Hall, East Lansing, MI 48824, USA.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0002-2034-3604; Barua pepe ya mawasiliano: ngonyani@msu.edu

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*21 Novemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Mofolojia Mshikanisho, Mofolojia Isoshikanisho, Mofimu, Kiolezo, Ruwaza.*

**IKISIRI**

Makala hii inafafanua na kujadili mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili na dhana ya mofimu. Baada ya kuelezea sifa bainifu za mofolojia mshikanisho na isoshikanisho, mifano kadha ya mofolojia hiyo katika Kiswahili inafafanuliwa. Mifano hiyo ni katika vionyeshi, uradidi, na ufupishaji wa majina na nomino. Violezo na ruwaza vinaelezwa kuwa muhimu katika fasili ya mofimu katika mofolojia isoshikanisho. Makala inabainisha mofimu za Kiswahili zinaundwa na vipandesauti na violezo. Kwa upande mwingine, violezo hivyo na mifano ya vifupisho vya majina kuwa silabi mbili inabainisha dhima kubwa ya arudhi na katika kuunda maneno ya Kiswahili.

**APA CITATION**

Ngonyani, D. (2023). Mofolojia Isoshikanisho katika Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(2), 15-29. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580.

**CHICAGO CITATION**

Ngonyani, Deo. 2023. "Mofolojia Isoshikanisho katika Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (2), 15-29. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580.

**HARVARD CITATION**

Ngonyani, D. (2023) "Mofolojia Isoshikanisho katika Kiswahili", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), pp. 15-29. doi: 10.37284/jammk.6.2.1580.

**IEEE CITATION**

D. Ngonyani "Mofolojia Isoshikanisho katika Kiswahili", *EAJSS*, vol. 6, no. 2, pp. 15-29, Nov. 2023.

**MLA CITATION**

Ngonyani, Deo. "Mofolojia Isoshikanisho katika Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 2, Nov. 2023, pp. 15-29, doi:10.37284/jammk.6.2.1580.

## UTANGULIZI

Mofolojia ya Kiswahili na lugha za Kibantu kwa ujumla huchukuliwa kama mfano bora wa mofolojia ya mshikanisho. Mofolojia mshikanisho huhusisha mizizi na viambishi awali na viambishi tamati navyo hutungwa pamoja mithili ya shanga kwenye uzi (Spencer, 1991; McCarthy, 1981; Bye & Svenonius, 2012). Vipandesauti mbalimbali hutambuliwa kuwa mofimu kwa kuwa vinaonekana tena na tena katika nafasi ileile katika maneno. Mfano wa mofolojia mshikanisho ni kitenzi hiki cha Kiswahili.

(1) Tu-li-po-m-fung-ul-ish-a

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

Kitenzi hiki kimejengwa kutokana na mzizi **fung**. Viambishi awali vya kiima (**tu-**), njeo (**li-**), kielezi (**po-**), na yambwa (**m-**) vinautangulia mzizi huo. Viambishi tamati vya kutendua (**-ul**), kutendesha (**-ish**), na kiambishi tamati (**-a**) vinakamilisha kitenzi hicho. Mofolojia ya kitenzi hiki inaonesha vipandesauti vinavyounda mofimu na mipaka dhahiri ya mofimu, na kila mofimu ikiwakilisha maana fulani. Mofimu zimepangwa katika msitari na zinaweza kutambuliwa katika mfuatano wake.

Picha hii sahili inaficha utangamani wa mofolojia ya Kiswahili na lugha za Kibantu. Katamba (1978) na Kosch (2005), kwa mfano, wanathibitisha kwamba kuna mofolojia katika lugha za Kibantu ambayo si ya mshikanisho. Wataalamu wa isimu tarakilishi pia wanatambua kuwepo kwa mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu (Hurskainen, 2005). Kwa mfano, kivumishi cha pekee katika Kiswahili kinaonesha dhahiri kwamba si mofolojia yote ya Kiswahili ni sahili au mshikanisho, kama mifano hii inavyoonesha.

(2) kitabu chochote
mti wowote
mambo yoyote
pahali popote

Mifano hii inaonesha mambo kadha ambayo yanakinzana na sifa bainifu za mofolojia mshikanisho. Kwanza, tunaona fonimu tofauti tofauti zinaoneka katika mazingira yaleyale ya kifonolojia. Kivumishi kinaonekana kuwa na umbile la **_o_ote**. Ndiyo kusema ni mofimu katizwa. Pia kina upatanisho wa kisarufi kwa nomino iliyotangulia. Lakini mofimu ya upatanisho pia ni mofimu katizwa. Kwa mfano **ch-ch-**. Shina na pia kiambishi vinaonekana katika maumbo ya uradidi, maumbo ambayo ni ya mofolojia isoshikanisho. Aina hii ya mofolojia haijapata kuwavutia wanaisimu wengi wa Kiswahili ijapokuwa ina mambo mengi ya kutufundisha.

Makala hii inachambua maumbo kadha yenye kudhihirisha mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili. Uchambuzi huu utapelekea kuyaelezea baadhi ya maumbo kuwa yanajengwa kwa kutumia violezo ambavyo ni vya kiarudhi. Makala inaangazia maswali matatu:

- Ni mofolojia gani isoshikanisho iliyo katika Kiswahili?
- Ni mali ghafi gani zinazotumika kuunda mofimu za Kiswahili katika mofolojia isoshikanisho?
- Ni nini dhima ya arudhi katika kuunda maneno ya mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili?

Makala inatalii maswali haya katika sehemu 4 zifuatazo. Sehemu ya pili ya makala inafafanua sifa bainifu za mofolojia mshikanisho na mofolojia isoshikanisho. Sifa hizo zitadhihirika katika maumbo ya vionyeshi, uradidi, na ufupishaji wa majina katika sehemu ya 3. Sehemu ya 4 inaelezea nafasi ya arudhi katika uundaji wa maneno ya Kiswahil. Sehemu ya 5 ni ya muhtasari na hitimisho.

## MOFOLOJIA ISOSHIKANISHO

Sehemu hii ya makala inafafanua na kuorodhesha sifa zinazopambanua mofolojia mshikanisho kutoka mofolojia isoshikanisho. Bye & Svenonius (2012) na Spencer (1991) wanaorodhesha sifa bainifu za mofolojia mshikanisho. Sifa hizo zinapokosekana ndipo tunapopata mofolojia isoshikanisho. Kwa kutumia sifa hizo makala inadhihirisha kwamba sehemu kubwa ya mofolojia ya Kiswahili ni mofolojia mshikanisho, lakini pia iko mofolojia isoshikanisho.

Sifa ya kwanza ya mofolojia mshikanisho ni mpangilio wa mofimu katika mfuatano wa ulalo au msitari. Maneno hujengwa kwa kuongeza mofimu kabla ya shina au baada ya shina. Turejee mifano wa vitenzi na nomino za Kiswahili.

(3) a. wa-li-o-wa-pig-an-i-a
b. ki-vut-i-o

Katika mfano (3a), kitenzi hicho kimeundwa kutokana na mzizi **pig**. Mzizi huu ulinyambuliwa na mofimu ya kutendana **-an**, na ya kutendea **-i** na kiambishi tamati **-a**. Pia, viambishi awali vya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580


kiima **wa-**, njeo **li-**, kiambishi cha urejeshi **o-**, na kiambishi cha yambwa **wa-**. Neno lililo katika (3b) limeundwa kwa kutumia mzizi **vut**. Mzizi huu umenyambuliwa na kauli ya kutendea **-i**, na kiambishi cha unominishaji **-o**. Nomino hii imepata kiambishi awali **ki-** kuashiria ngeli. Viambishi vyote vimeongezwa kwenye mzizi na vinaonekana kimoja baada ya kingine.

Mifano hii inatoa vielelezo pia vya sifa ya pili ya mofolojia mshikanisho. Sifa hiyo ni mshikamano wa kila mofimu. Kila mofimu ni kipande kimoja kisichogawanyika au kukatizwa chenye kipandesauti kimoja au zaidi. Kwa hivyo, katika mfano (3a), hakuna kipande kinachooneka kugawanyika na kuwa katika sehemu mbili ilhali ni mofimu moja. Mzizi, kwa mfano, unaundwa na vipandesauti vitatu /pig/.

Sifa hizo mbili zinadhihirisha sifa bainifu ya tatu. Sifa hiyo ni kwamba mofolojia hiyo inaundwa kwa kujenga kutoka kiini au mzizi unaounda msonge. Mofimu huonekana kuongezwa hatua kwa hatua kutoka kiini. Kwa mfano, neno la (3b), linaweza kuoneshwa kama hivi katika (4b).

(4) a. kivutio

b.





Mchoro matawi huu unakusudia kufafanua kwamba neno **kivutio** linaundwa na mzizi **vut** ambao ni kitenzi. Kitenzi hiki kimenyambuliwa na kiambishi cha kutendea **-i** na kufanya **vuti**. Baada ya hapo, shina hili limenyambuliwa na kuwa **vutio,** ambayo ni nomino. Na kila nomino inaainishwa katika ngeli. Ishara moja ya ngeli ni kiambishi kama **ki-** kilicho hapo.

Vitenzi vya lugha za Kibantu vimechanganuliwa kuwa vya msonge pia ambao una matawi mengi zaidi ya nomino. Twaweza kutumia kielelezo tawi cha Myers (1998) alichotumia kuchanganua vitenzi vya Chishona. Hapa mfano wa Kiswahili unatumika kuleta picha ya muundo huo.

(5) a. tu-li-m-fung-i-a

b.




 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

Kitenzi chenye njeo kina vipashio viwili. Kipashio kimoja, shina kuu, kina mzizi kama kiini chake. Kipashio cha pili, kisaidizi, kina njeo kama kiini chake. Shina kuu lina muundo wa msonge ndani yake unaoakisi jinsi kitenzi kilivyonyambuliwa.

Uchambuzi huu ulitokana hasa na hoja za kifonolojia kama vile uradidi na toni, na za kimofolojia kama miundo ya urejeshaji. Muundo huu wa kitenzi unaonekana kukubalika na wachunguzi wengine kama vile Barrett-Keach (1986), Mchombo (2004), na Ngonyani (2006). Kwa kifupi, muundo wa kitenzi cha Kiswahili ni mfano mzuri wa muundo wa msonge wa mofolojia mshikanisho. Kitenzi kinajengwa msonge kutoka kwenye kiini chake yaani mzizi.

Mifano tuliyoiangalia hapa inapelekea sifa bainifu ya nne. Sifa hiyo ni kuwa uundaji wa maneno huongeza vipande au mofimu. Mofolojia shikanisho haipunguzi vipande katika uambishaji au unyambuaji. Wala mofolojia hiyo haibadilishi sauti za ndani ya mofimu. Katika Kiingereza, kwa mfano, tunaona maneno nama /siŋ/ `imba' na kwa wakati uliopita neno linabadilika na kuwa /sʌŋ/. Kipandesauti cha ndani kimebadilishwa na kuufanya mzizi kuwa una sehemu mbili zisizo pamoja, kinyume na sifa ya pili tuliyoiona hapo juu.

Sifa ya tano ya mofolojia mshikanisho ni kutoruhusu mofimu ya nje kuteua mofimu ya ndani ya mzizi. Vimbishi huongezwa mbele na na nyuma ya shina au mzizi. Hakuna uchopekaji ambao utaufanya mzizi kuwa mofimu katizwa (Bye & Svenonius 2012, Spencer 1991).

Katika mifano ya Kiswahili niliyotoa hapo juu ni dhahiri kwamba sifa moja kuu nyingine ya sita ni kuwa maneno huweza kugawanywa katika vipande vinavyoundwa na vipandesauti. Maumbo ya maneno na vipashio vyenye kuleta maana vinaundwa kwa vipandesauti tu.

Kwa kuzingatia sifa bainifu zilizofafanuliwa hapa, twaweza kusema kwamba mofolojia isoshikanisho ni ile ambayo haisadifu sifa hizi. Kwa kifupi, mofolojia isoshikanisho (Bye & Svenonius, 2012; Spencer, 1991):

- Haifuati ulalo au msitari. Maumbo ya maneno yanaweza kuwa ya mwingiliano wa vipandesauti vya mofimu tofauti.
- Mofimu hazina mshikamano. Mofimu moja inaweza kugawika katika vipande sauti viwili au zaidi. Mofimu katizwa na uchomekaji ni mifano mizuri.
- Muundo wake si wa msonge na unaweza kukosa kiini. Mofolojia ya lugha za Kisemitiki, kwa mfano, inaonesha mwingiliano wa mofimu ambazo haziundi msonge.
- Mofimu zinaweza kuundwa kwa kupunguza vipandesauti au kwa kubadilisha sehemu ya ndani ya mzizi au shina. Ufupishaji wa maneno ni mfano mzuri.
- Mofimu ya ndani huweza kuteuliwa na mofimu ya nje.
- Mofimu inaweza kuwa kiolezo tu na si vipandesauti. Violezo ni nafasi za maumbo ambazo zinatakiwa kujazwa na vipandesauti.

Mfano mmoja unaoonesha sifa hizi za mofolojia isoshikanisho ni wa mofolojia ya Kiarabu. Kiarabu ni lugha yenye muundo tofauti sana na muundo wa Kibantu. Mofolojia ya Kiarabu hutolewa kama mfano wa muundo unaojengwa kwa mizizi na violezo. Katika mifano ifuatayo, mizizi ya vitenzi inaoneshwa kuwa ni ya konsonanti tatu mbalimbali. Hizo zinatajwa hapa kama XYZ. Yaani, konsonanti ya kwanza ni X, ya pili ni Y, ya tatu ni Z. Ili kuambisha au kunyambulisha, basi kuna violezo vinataja ni mfuatano wa namna gani wa konsonanti na irabu, na ni irabu gani zitumike.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

**Jedwali 1: Mofolojia ya Kiarabu**

| | A | B | C | Kiolezo |
|---|---|---|---|---|
| a. | darasa `alijifunza’ | hamala `alibeba’ | rasama `alichora’ | XaYaZa |
| b. | darrasa `alifundisha’ | hammala `alipakia’ | rassama `alichoresha’ | XaYYaZa |
| c. | darraasun `mwanafunzi’ | hammaalun ‘mpagazi’ | rassaamun `mchoraji’ | XaYYaaZun |
| Mzizi | drs | hml | rsm | |


**Chanzo**: (Kenstowicz, 1994)

Katika mifano hii, mizizi mitatu inaoneshwa nayo ni **drs** `kujifunza’, **hml** `kubeba’, na **rsm** `kuchora.’ Ili kupata `alibeba’, kwa mfano, kitenzi **hml** `kubeba’ kinatumika. Njeo ya wakati uliopita na pia kiima cha nafsi ya tatu umoja inachomeka **a-a-a**. Unyambulishaji wa kutendesha unadai mfuatano au kiolezo cha XIYYIZI. Njeo ya **-a-a-a** inachomekwa

Mofimu tunazoziona hapa hazioneshi mshikamano bali zinaingiliana kwa mujibu wa violezo. Mzizi wenye konsonanti tatu unachomekwa irabu na pengine nafasi zaidi za konsonanti. Kiolezo kama XaYYaZa kinadhihirisha kwamba si mofimu zote ambazo ni za vipandesauti. Hapa mofimu ni kiolezo chenyewe kinachodai kuwa na konsonanti ngapi na irabu ngapi. Mofolojia inawakilishwa kwa kutumia rusu tatu: Mzizi unaunda rusu moja (mingi ya mizizi ikiwa ya konsonanti tatu). Rusu nyingine ni ya kiolezo chenye kuonyesha mfuatano wa nafasi za konsonanti na irabu (KIKIK au KIKKIK). Rusu ya tatu ni ya irabu, katika mifano hii ni njeo. Rusu hizo zinaoneshwa katika mifano hii miwili.

(6) Mofolojia ya vitenzi vya Kiarabu (McCarthy, 1981)

a. **katab** ‘aliandika’ b. **kattab** ‘aliandikisha’




Kwa kuzingatia rusu tatu hizo, tunaona kwamba muundo wa maneno hayo ya Kiarabu si mshikanisho. Mzizi hauna mshikamano, unachomekwa irabu za ngeli. Muundo huu wa maneno hauwezi kuwasilishwa kwa msonge kwa sababu maneno hayajengwi kutoka kwenye kiini na kuongeza tu. Kila kiolezo kina maana maalum na vipandesauti pia vina maana yake. Kwa hivyo basi, mofolojia hii ni mfano wa mofolojia isoshikanisho na ni tofauti sana na mofolojia ya vitenzi na nomino za Kiswahili na Kibantu kwa ujumla.

Uwasilishaji huu wa mofolojia ya Kiarabu ulitokea kufuatia maendeleo katika utafiti wa fonolojia, hususan, nadharia ya Vipandesauti Huru (Goldsmith, 1976; Leben, 1973; Massamba, 1982). Somo moja muhimu lililotokana na nadharia hiyo ni kwamba uwakilishi wa kifonolojia waweza kuoneshwa katika rusu zilizo huru. Vipengele kama vipandesauti, toni, vipambasauti kila kimoja kina rusu yake. Ushahidi wa toni na mifanyiko mbalimbali ya toni ulidhihirisha kwamba toni inaweza kuwa kipengele huru na si sehemu ya sifa za

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

vipandesauti. Ugunduzi huu uliwawezesha wanamofolojia nao kuwasilisha mofolojia isoshikanisho kwa kupendekeza rusu za kimofolojia.

Kwa muhutasari, sehemu hii ya makala imefafanua sifa bainifu za mofolojia mshikanisho na mofolojia isoshikanisho. Mifano kutoka Kiswahili imetumika kufafanua mofolojia mshikanisho. Na kwa hakika, sehemu kubwa ya mofolojia ya Kiswahili ni mshikanisho. Hata hivyo, ipo baadhi ya miundo ambayo inavunja mfumo wa ushikanisho ambao unatawala zaidi katika lugha za Kibantu. Miundo hiyo inafafanuliwa katika sehemu ifuatayo.

## MOFOLOJIA ISOSHIKANISHO KATIKA KISWAHILI

Sehemu hii ya makala inatoa mifano mitatu ya miundo ya maneno inayotokana na mfumo usoshikanisho. Mifano hiyo ni:

- Violezi vya vionyeshi
- Uradidi
- Ufupishaji wa majina na nomino

Kila moja itaoneshwa kutokidhi sifa bainifu za mofolojia mshikanisho, bali huundwa kwa kufuata violezo na ruwaza.

### Mofolojia ya Vionyeshi

Vionyeshi vya Kiswahili vyatambuliwa kuwa vinaakisi umbali au ukaribu wa namna tatu inavyopambanuliwa na msemaji (Kihore na wenzake, 2009). Vionyeshi hivyo ni:

- Vionyeshi vya ujirani
- Vionyeshi vya kati
- Vionyeshi vya mbali

Vionyeshi vya ukaribu vinatumika hasa kuonesha vitu vilivyo karibu na msemaji, ilhali vionyeshi vya umbali huonesha vitu vilivyo mbali na msemaji na msemewa (Kihore na wenzake, 2009). Vionyeshi vya kati vinatumika kwa vitu vilivyo mbali na msemaji, bali vinaweza kuwa karibu na msemewa.

**Jedwali 2: Mfano wa vionyeshi vya mtoto**

| | | Uhusianishorejeshi |
|---|---|---|
| **Ujirani** | Mtoto huyu | Karibu na msemaji |
| **Kati** | Mtoto huyo | Karibu na msemewa |
| **Mbali** | Mtoto yule | Mbali na msemaji na msemewa |

Kama ilivyo katika vipashio vingine vingi, maana za umbali zinazotajwa si lazima ziwe zikirejea umbali kiuhalisia. Kionyeshi cha kati, kwa mfano hutumika sana kuashiria kwamba nomino au kirai nomino kilikwisha tajwa katika muktadha wa matini. Kwa kuwa makala hii inajikita zaidi katika muundo, haitajadili zaidi kuhusu maana za vionyeshi wala kutoa maelezo ya kipragmatiki. Badala yake itafafanua na kuchambua muundo wa vionyeshi hivyo.

Vionyeshi vinachukua maumbo mbalimbali ya kifonimu kulingana na ngeli na nomino inayovumishwa. Kwa kuanza, inafaa kuorodhesha viwakilishi kwa mujibu wa ngeli zote katika Kiswahili.

**Jedwali 3: Vionyeshi vya Kiswahili**

| Ngeli | Nomino | Karibu | Kati | Mbali |
|---|---|---|---|---|
| 1 | mtoto | huyu | huyo | yule |
| 2 | watoto | hawa | hao | wale |
| 3 | mti | huu | huo | ule |
| 4 | miti | hii | hiyo | ile |
| 5 | gazeti | hili | hilo | lile |
| 6 | magazeti | haya | hayo | yale |
| 7 | kitabu | hiki | hicho | kile |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

| Ngeli | Nomino | Karibu | Kati | Mbali |
|---|---|---|---|---|
| 8 | vitabu | hivi | hivyo | vile |
| 9 | nyumba | hii | hiyo | ile |
| 10 | nyumba | hizi | hizo | zile |
| 11 | ukuta | huu | huo | ule |
| 10 | kuta | hizi | hizo | zile |
| 12 | uhuru | huu | huo | ule |
| 14 | kucheka | huku | huko | kule |
| 16 | nyumbani | hapa | hapo | pale |
| 17 | nyumbani | huku | huko | kule |
| 18 | nyumbani | humu | humo | mle |

Mifano hii inadhihirisha muundo wa vionyeshi ambao si wa mshikanisho. Vionyeshi vya karibu vina fonimu moja /h/ inayooneka kwa ngeli zote. Kwa hivyo muundo wake unaanza kwa mpaka huu, kama inavyooneshwa hapa.

(7) h-uyu
h-awa
h-uu
h-ii
h-ili
h-iki
h-aya

Pengine uchambuzi bora zaidi ni ule unaoonesha mpaka wa mofimu baada ya silabi ya kwanza. Kihore na wenzake (2009) na Wesana-Chomi (2013), kwa mfano, wanayagawa maneno hayo kama **hu-yu, ha-wa, hu-u, hi-li**, na kadhalika. Uchambuzi huu unaelekea kupendekeza kuwa **hu-, ha-**, na **hi-** kuwa ni alomofu za mzizi. Lakini irabu ipi kati ya hizo tatu itumike ni jambo ambalo linaamuliwa na nomino inayotawala upatanisho wake kama vile ambavyo sehemu ya mwisho kama **-wa, -yu, -u, -li, -pa**, na kadhalika.

Kitu ambacho ni dhahiri kabisa ni kwamba kionyeshi hiki kinaundwa kwa silabi mbili. Silabi ya pili ndiyo inayoonesha upatanisho wa kisarufi wa dhahiri zaidi. Silabi hiyo ni kama ile inayoonekana katika upatanisho wa kisarufi wa kiima, kama inavyooneshwa hapa.

**Jedwali 4: Upatanisho wa kisarufi wa kiima**

| Ngeli | Nomino | Kitenzi |
|---|---|---|
| 1 | mtoto | alianguka* |
| 2 | watoto | walianguka |
| 3 | mti | ulianguka |
| 4 | miti | ilianguka |
| 5 | gazeti | lilianguka |
| 6 | magazeti | yalianguka |
| 7 | kitabu | kilianguka |
| 8 | vitabu | vilianguka |
| 9 | nyumba | ilianguka |
| 10 | nyumba | zilianguka |
| 11 | ukuta | ulianguka |
| 10 | kuta | zilianguka |
| 12 | uhuru | ulipatikana |
| 14 | kucheka | kulikoma |
| 16 | nyumbani | palichafuka |
| 17 | nyumbani | kulifikia |
| 18 | nyumbani | mlichafuka |

Tukiachia ngeli ya kwanza ambayo inahitaji maelezo tofauti (**huyu**), kiambishi cha kiima ndicho hicho hicho kinachoonekana kwenye kionyeshi cha ujirani. Kwa mfano katika **magazeti yalianguka**, kiambishi cha kiima ni **ya-**. Kiambishi **ya-** ndicho kinachoonekana katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580


**magazeti** **haya**. Silabi ya kwanza ya kionyeshi ina mwanzosilabi /h/ na inanakili irabu ya silabi ya upatanisho. Kwa hivyo irabu /a/ ni kwa **magazeti haya**. Ruwaza hii inajirudia kwa ngeli zote.

Kwa hivyo, kwa kifupi, kionyeshi cha ujirani kinaundwa kwa kiolezo chenye sifa hizi:

- Silabi mbili (σ σ)
- Mwanzo wa silabi ya kwanza ni /h/
- Silabi ya pili ni ya upatanisho wa kisarufi
- Kiini cha silabi ya kwanza kinanakili kiini cha silabi ya upatanisho wa kisarufi.

Kiolezo hicho kinaweza kuwasilishwa hivi:


(8)




Kiolezo hiki kinaonesha nafasi tatu ambazo vipandesauti vyake havijaorodheshwa na ambavyo vitatokana na upatanisho wa kisarufi. Silabi ya upatanisho wa kisarufi si lazima iwe na konsonanti ya mwanzo.

Vionyeshi vya kati vina muundo ambao unabadilisha vipandesauti vya kati ilhali vipendesauti vya mwanzo na mwisho ni vilevile kwa ngeli zote. Kionyeshi hicho ni **h__o**. Sehemu ya kati ndiyo ya upatanisho wa kisarufi. Kiolezo chake kina silabi mbili kama inavyoonekana kwenye kielelezo hiki.


(9)




Umbo hili linashabahiana na lile la kionyeshi cha ujirani isipokuwa badala ya irabu ya upatanisho wa kisarufi mwishoni kuna **-o**. Iwapo mzizi utachukuliwa kuwa ni **h__o**, basi ni dhahiri kwamba ni mofimu katizwa isiyokuwa na mshikamano. Kiolezo cha kionyeshi cha kati ni mfano mzuri wa mofolojia isoshikanisho kwa sababu kinaonekana dhahiri kuwa ni cha mofimu katizwa. Vipandesauti vya upatanisho wa kisarufi vinachomekwa kati ya **h** na **o** kama viambishindani.

Vionyeshi vya mbali vina silabi mbili pia. Silabi ya pili inasomeka **le** na ya kwanza inatokana na upatanisho wa kisarufi.

(10)




Kionyeshi hiki cha umbali kinaundwa na kiolezo pia lakini kinaoneka kuwa na sifa za mshikanisho.

**Uradidi**

Uradidi ni mchakato wa kuunda maneno unadhihirika kwa kurudia neno au sehemu ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

neno (Inkelas & Downing, 2015; Wiltshire & Marantz, 2000). Mada hii imewavutia wanaisimu wengi wakiwemo wanaisimu wanaochunguza lugha za Kibantu kikiwemo Kiswahili (Hannah & Yoneda, 2018; Novotna, 2000)  Wachunguzi hao wanatambua kuwepo kwa kiolezo ambacho hakina vipandesauti, bali hupata kujazwa na vipandesauti vya neno chanzo.

Kuna vyanzo vya vipandesauti vya aina mbili: (a) vipandesauti vya maneno, na (b) vipandesauti vinavyotokana na upatanisho wa kisarufi. Mfano mzuri wa vipandesauti vya maneno vinavyorudia ni katika uradidi wa vitenzi kama hivi (11) na (12).

(11) a. wa-li-kata-kata
b. wa-li-vi-kata-kata

(12) a. wa-li-vyo-vi-zungusha-zungusha
b. wa-li-vyo-m-zungushia-zungushia

Katika mifano hii, ni dhahiri kwamba mashina ya vitenzi ndiyo yanayorudiwa. Viambishi awali vya upatanisho, njeo, kiima, na urejeshaji havirudiwi. Bali mashina yenye mzizi na vinyambulisho vya kutendea, kutendesha, na kadhalika hurudiwa. Mchakato huu unajulikana sana katika lugha za Kibantu na katika Kiswahili hutumika hasa kwa kuonesha marudio ya kitendo, mwendelezo wa kitendo, utendaji wa ovyo, na hata kukazia kitendo (Ashton, 1947; Hannah & Yoneda, 2018; Inkelas & Downing, 2015; Novotna, 2000). Maelekezo ya uradidi huu ni kunakili shina lote.

Uradidi unaotumia mali ghafi kutoka upatanisho wa kisarufi ni tangamani zaidi kwa sababu kuna mambo kadha yanayohusika. Kwanza, kiolezo chake kinataja muundo wa kiarudhi. Pili, vipandesauti vinavyotumika havitoki moja kwa moja kutoka kwa neno fulani bali katika dhahania ya upatanisho wa kisarufi wa nomino inayohusika (Inkelas & Downing, 2015; Wiltshire & Marantz, 2000). Hapo awali tuliona violezo vya vionyeshi ambavyo tulibaini vinatumia vipandesauti vya upatanisho wa kisarufi. Uradidi mmojawapo tuupatao ni ule wa vionyeshi kama inavyoonekana katika jedwali.

**Jedwali 5: Uradidi wa vionyeshi vya kati**

| Ngeli | Mfano | h-o+h-o |
|---|---|---|
| 1 | mtoto | huyohuyo |
| 2 | watoto | haohao |
| 3 | mlango | huohuo |
| 4 | milango | hiyohiyo |
| 5 | jiwe | hilohilo |
| 6 | mawe | hayohayo |
| 7 | kikapu | hichohicho |
| 8 | vikapu | hivyohivyo |
| 9 | nyumba | hiyohiyo |
| 10 | nyumba | hizohizo |
| 11 | ukuta | huohuo |
| 14 | uzuri | huohuo |
| 15 | kucheka | hukohuko |
| 16 | nyumbani | hapohapo |
| 17 | nyumbani | hukohuko |
| 18 | nyumbani | humohumo |

Uradidi huu unaundwa na kiolezo kinachotaka kurudiwa kwa silabi mbili kukiwa na vipandesauti vinne ambavyo vimetajwa **h__o-h__o**. Sehemu ya kiolezo iliyo wazi ndiyo inayojazwa na vipandesauti kutokana na upatanisho wa kisarufi kama tulivyoona kwenye vionyeshi hapo awali. Vionyeshi vyote vitatu vinaweza kufanya uradidi huu kusisitiza au kutambulisha nomino inayohusika. Kwa mfano:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.


East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 2, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

(13) a. kitabu hikihiki
kitabu hichohicho
kitabu kilekile

b. nyumbani hapahapa
nyumbani hapohapo
nyumbani palepale

Kiolezo ni kilekile cha silabi mbili za kionyeshi ambazo zinarudiwa na kwa hivyo kufanya silabi nne. Huu ni mfano wa uradidi kamili, ambapo chanzo kizima hurudiwa.

(14)




Hapa kionyeshi cha kati ndiyo chanzo cha uradidi. Kama ilivyoelezwa mwanzo, chanzo hicho kina mofolojia isoshikanisho.

Uradidi usio kamili unaonekana katika vivumishi vya pekee. Katika maneno haya, kiolezo kinatumia arudhi na vipandesauti nafasi mbili za konsonanti ambazo ndizo zinazorudiwa. Vipandesauti na mapengo vinaweza kuoneshwa hivi **_o_ote**. Chanzo cha kivumishi hiki ni kivumishi cha kiasi **_ote**. Nafasi ya kwanza ya konsonanti hutokana na upatanisho wa kisarufi. Uradidi wa **_o_ote** kwa kweli hurudia silabi ya kwanza ya kivumishi hicho cha kiasi. Orodha nzima ya viwakilishi vya muundo huu vinaoneshwa katika jedwali.

**Jedwali 6: Uradidi wa kiwakilishi cha pekee**


| Ngeli | Mfano | KoKote |
|---|---|---|
| 1 | mtoto | yeyote |
| 2 | watoto | wowote |
| 3 | mlango | wowote |
| 4 | milango | yoyote |
| 5 | jiwe | lolote |
| 6 | mawe | yoyote |
| 7 | kikapu | chochote |
| 8 | vikapu | vyovyote |
| 9 | nyumba | yoyote |
| 10 | nyumba | zozote |
| 11 | ukuta | wowote |
| 10 | kuta | zozote |
| 14 | uzuri | wowote |
| 15 | kucheka | kokote |
| 16 | nyumbani | popote |
| 17 | nyumbani | kokote |
| 18 | nyumbani | |

Kiolezo cha uradidi huu kinaweza kuwakilishwa hivi:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

(15)




Mofolojia ya viwakilishi vya pekee si msikanisho kwa sababu mofimu ina mapengo kwa hivyo inakosa mshikamano na viwakilishi hivi vinaundwa na kiolezo cha uradidi.

Kwa kuhitimisha, uradidi unaoonekana katika Kiswahili ni mfano mmoja wa mali ghafi inayotumika kuunda vipashio tuviitavyo mofimu. Mali ghafi hizo ni mchakato wa kurudia na violezo. Mchakato na violezo hutumia vipandesauti, bali vyenyewe si vipandesauti.

**Ufupishaji wa Majina na Nomino**

Ufupishaji wa majina ni mfano wa mofolojia isoshikanisho kwa sababu unapunguza vipande sauti vinavyounda mzizi au jina kamili. Katika Kiswahili, majina kadha yamepata vifupisho kama namna mbadala ya kuyatamka. Mifano michache inatosha kuonesha mfanyiko huu.

(16)

| | |
|---|---|
| Ramadhani | Rama |
| Mohamedi | Medi |
| Rafaeli | Rafa |
| Abdulla | Dula |
| Emmanueli | Manu |
| Gloria | Gilo |
| Zeituni | Tuni |
| Selemani | Sele |
| Sikujua | Siku |

Majina ya kigeni yaliyokopwa kadhalika ya Kibantu au ya Kiswahili kiasili hufupishwa kama inavyoonekana kwenye mifano hiyo.

Ufupishaji huu hauishii katika majina halisi tu bali unaonekana pia katika nomino mbalimbali kwa mfano nomino hizi za misimu kutoka Reuster-Jahn & Kiessling (2006).

(17)

| | |
|---|---|
| kondakta | konda |
| Studenti | denti |
| dereva | dere |
| usukani | suka |
| shemeji | shemu |
| kondomu | ndomu |
| pajero | jero |
| bunduki | nduki |

Ijapokuwa kanuni inayoteua sehemu kinakotoka kifupisho haiko dhahiri, umbo la kifupisho ni dhahiri kabisa. Vifupisho vyote vinaonekana kuundwa kutokana na silabi mbili.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

**Jedwali 7: Muundo wa vifupisho**

| Shina | Kifupisho | Muundo wa kifupisho | Kilichoondolewa |
|---|---|---|---|
| kondakta | konda | σ́ σ | σ |
| studenti | denti | σ́ σ | σ |
| usukani | suka | σ́ σ | σ σ |
| Mohamedi | Medi | σ́ σ | σ́ σ |
| Emanueli | Manu | σ́ σ | σ σ σ |
| Sikujua | Siku | σ́ σ | σ σ |

Vifupisho vimetoka mwanzo, katikati, na hata mwishoni mwa mashina. Sehemu zilizoondoshwa zinaweza kuwa silabi moja, mbili, tatu, au zaidi. Vifupisho vina silabi mbili, cha kwanza kikipewa mkazo, na hicho ndicho kiolezo cha vifupisho. Mchakato wa kimofolojia unaoondoa vipandesauti ni moja ya michakato ya mofolojia isoshikanisho.

Mifano iliyojadiliwa katika sehemu hii inaonesha violezo vya vionyeshi, uradidi mbalimbali, na pia katika kufupisha majina au nomino. Kwa hivyo basi, violezo ni dhana muhimu sana katika kuchunguza mofolojia isoshikanisho, jambo linalojadiliwa katika sehemu ifuatayo.

## MOFIMU, VIOLEZO NA ARUDHI

Ufafanuzi wa mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili unaibua mambo kadha katika nadharia ya mofolojia. Sehemu hii ya makala itaangazia fasili ya dhana ya mofimu na nafasi ya arudhi katika mofolojia isoshikaniso katika Kiswahili.

Ufafanuzi uliotolewa hapa unatudai tufasili mofimu kwa kina zaidi. Wanaisimu wanaozungumzia mofolojia ya Kiswahili aghalabu hufasiri mofimu kama kipashio kidogo kabisa cha maana (Kihore na wenzake, 2009; Matinde, 2012; Wesana-Chomi, 2013). Lakini endapo tutajiuliza mofimu ya kionyeshi cha karibu ni nini kama **huyu, hizi**, **hivi**, na **hapa**, hatuwezi kusema ni **h** peke yake. Fonimu hii peke ndiyo inayoonekana katika vionyeshi vyote. Sehemu iliyobakia inahusu upatanisho wa kisarufi. Kwa hivyo, hatuna budi kusema kwamba kionyeshi cha karibu kina kipandesauti **h** pamoja na nafasi nyingine tatu Irabu-Konsonanti-Irabu (**h**IKI). Hiki ni kiolezo cha silabi mbili ambacho kinachangia katika maana tunayozungumzia. Kwa hiyo, mali ghafi zinazounda mofimu hapa ni kipandesauti na kiolezo.

Violezo msingi mkubwa wa uradidi. Kwa mfano katika virai **mlango wowote** na **jambo lolote**, vivumishi pekee **wowote** na **lolote** vinaundwa na vipandesauti **-ote** na kiolezo. Kuna konsonanti (K) inayoashiria upatanisho wa kisarufi na pia kiolezo cha silabi kabla ya K**ote**. Silabi hii hujazwa vipandesauti kwa kutumia silabi ya kwanza ya Kote. Katika fasili ya mofimu inatupasa kujumuisha vipandesauti, violezo na mchakato mzima wa kunakili vipandesauti kutoka kwenye shina au chanzo chochote.

Dhana ya mchakato inahusika sana katika mofolojia isoshikanisho. Katika ufupisho wa majina na nomino, mchakato unaagiza kuondoa vipandesauti na kubakiza silabi mbili au egemeomkazo. Hakuna mabadiliko ya maana katika ufupisho. Kwa mfano, mtu anayeitwa **Sikujua** habadiliki anapoitwa **Siku**. Pengine muktadha wa kipragmatiki unaweza kuwa tofauti. Jina **Siku** litapatikana zaidi katika muktadha usio rasmi, na pengine linaweza kuashiria kufahamiana zaidi.

Fasili yetu ya dhana ya mofimu ni lazima izingatie pia vipandesauti huru kuwa miongoni mwa mali gafi ya mofimu. Mifano mizuri tunaipata katika lugha zenye kutumia toni. Mifano kutoka Kiigbo unafaa hapa.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

(18) Kiigbo (Emenanjo, 2015:112)

a. ákwá 'lia'
b. ákwà 'nguo'
c. àkwá 'yai'
d. àkwà 'kitanda'
e. ísí 'kichwa'
f. ísì 'harufu'

Katika mifano hii, tofauti ya maana baina ya maneno (a) – (d) na (e) – (f) inatokana na vipandesauti. Lakini maana baina ya maneno (a) hadi (d) haitokani na vipandesauti. Maneno hayo manne yana vipandesauti vilevile. Tofauti inatokana na toni. Neno lenye maana ya 'lia' (18a) lina tonijuu (J) katika silabi zote mbili (J J). Katika (18b), silabi ya kwanzi ni tonijuu, na ya pili ni tonichini (J C), na katika (18c) in C J. Kwa hivyo, tukirejelea swali letu la awali, je, ni nini kinachotufanya tupate maana tofauti katika data hizi za Kiigbo? Jibu letu lazima litaje vipandesauti (konsonanti na irabu) na vipandesautihuru (tonijuu na tonichini).

Tukijumuisha pia ufafanuzi wa data za Kiswahili zihusuzo mofolojia isoshikanisho, tunahitimisha kwamba mali ghafi ya mofimu ni:

- Vipandesauti ambavyo ni konsonanti na irabu
- Vipandesautihuru k.m. toni
- Violezo na ruwaza
- Mchakato k.m. uradidi na udondoshaji

Kategoria za kiarudhi zina dhima kubwa katika mofolojia isoshikanisho (McCarthy, 1981). Katika mifano iliyofafanuliwa hapo juu, silabi na egemeomkazo ni maumbo yanayofasili violezo mbalimbali. Nadharia ya Mofolojia ya Kiarudhi kama ilivyofafanuliwa na waasisi wake (McCarth, 1981; McCarthy & Prince, 1990; McCarthy & Prince, 1995) inaelezea jinsi ambavyo sifa za kiarudhi zinavyohusika katika maumbo ya maneno katika mofolojia isoshikanisho. Mkabala huu umetumika katika kuchanganua miundo ya mofimu katizwa kama ilivyo katika Kiarabu na lugha za nasaba na Kiarabu, viambishindani, uradidi, tabdili, na mofolojia ambazo zinaundwa kwa violezo.

(19) Msonge wa viunzi vya kiarudhi (McCarthy & Prince, 1995)

| | |
|---|---|
| Nn | (Neno la Kiarudhi) |
| \| | |
| E | (Egemeomkazo) |
| \| | |
| σ | (silabi) |
| \| | |
| μ | (mora) |

Kaida moja ya mofolojia arudhi ni: Violezo hubainishwa kwa kutumia vizio halisi vya kiarudhi: mora, silabi, egemeomkazo, na neno la kiarudhi. Violezo vinavyoonekana katika mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili vinaonesha vinapimwa kwa silabi, egemeomkazo, na neno la kiarudhi. Kiolezo cha ufupisho wa nomino na majina kinaonesha umuhimu wa egemeomkazo na pia kile kinachoelezwa kuwa umbile dogo kabisa la maneno ya Kiswahili, yaani silabi mbili (Park, 1997).

## HITIMISHO

Makala hii ilitalii dhana ya mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili na kujaribu kujibu maswali kuhusu mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili, mali ghafi za mofimu, na dhima ya arudhi katika kuunda maneno ya mofolojia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

isoshikanisho. Makala imefafanua mofolojia isoshikanisho katika vionyeshi ambavyo hutegemea violezo na baadhi yake ni mofimu katizwa, viwakilishi vya pekee vyenye kuundwa kwa kiolezo cha uradidi, uradidi kwa jumla ambao unafasiliwa kuwa na msingi wa violezo, na ufupishaji wa majina na nomino.

Ufafanuzi uliotolewa hapa umebaini kwamba mali ghafi zinazounda maneno na mofimu za Kiswahili ni (a) vipandesauti, (b) violezo na ruwaza, na (c) mchakato. Sehemu kubwa ya mofimu za Kiswahili inaundwa kwa vipandesauti. Yumkini jambo hili limepelekea kutozingatiwa kwa mali ghafi nyingine na maumbo yasoshikanisho. Vipandesauti peke yake vinaunda mofolojia shikanisho kama vinavyojidhihirisha katika vitenzi, nomino, na viwakilishi, ambayo ni sifa moja kubwa ya lugha za Kibantu. Violezo vinahusika pia katika muundo wa mofimu. Tumeona, kwa mfano, vionyeshi vya karibu vina kipandesauti kimoja tu ndicho kinachobainishwa pamoja na mapengo matatu ambayo hubainishwa kwa mfuatano wa Irabu-Konsonanti-Irabu (hIKI). Kuna maelekezo maalum ya kujaza nafasi hizo kwa mujibu wa upatanisho wa kisarufi.

Mifano miwili ya michakato katika mofolojia imejadiliwa. Mmoja ni uradidi na wa pili ni ufupishaji wa majina na nomino. Uradidi ni mfano mzuri wa mofolojia inayotumia mali ghafi za aina zote tatu zilizotajwa hapa kwa sababu unatokana na maelekezo ya mchakato kurudia vipandesauti vya neno au sehemu ya neno na pia kurudia huko lazima kufuate violezo.

Mofolojia isoshikanisho katika Kiswahili imesheheni malekezo ya maumbo yanayozingatia muundo wa silabi. Violezo vimejengwa kwa silabi na vifupisho vya majina na nomino vinazingatia umbile dogo la maneno ambalo ni silabi mbili. Ijapokuwa nafasi ya mofolojia isoshikanisho si kubwa sana katika muundo wa maneno ya Kiswahili kitipolojia, bado inafunza mengi kuhusu dhima ya silabi na arudhi katika lugha.

**MAREJELEO**


Ashton, E. O. (1947). *Swahili Grammar (Including Intonation)*. London: Longmans, Green and Co.

Barrett-Keach, C. (1986). Word-internal evidence from Swahili AUX/Infl. *Linguistic Inquiry, 17*(3), 559-564.

Bye, P., & Svenonius, P. (2012). Non-concatenative morphology as epiphenomeno. Kwenye J. Trommer (Mhar.), *Morphology and Phonology of Exponence : Morphology and Phonology of Exponence*. Oxford: Oxford University Press.

Emenanjo, E. N. (2015). *A Grammar of Contemporary Igbo: Constituents, Features and Processes*. Port Harcourt: M and J Grand Orbit Communications.

Goldsmith, J. (1976). *Autosegmental Phonology*. MIT: Tasnifu ya Uzamivu.

Hannah, G., & Yoneda, N. (2018). Functions of verb reduplication and verb doubling. *Jouranl of Asian and African Studies, 96*, 5-27.

Hurskainen, A. (2005). Solutions for handling non-concatenative processes in Bantu languages. Kwenye L. Arppe, L. Carlson, Lindén, Krister, J. Piitulainen, M. Souminen, Vainio, Martti, . . . Yli-Jyrä, Anssi (Wahar.), *Inquiries into Words, Constraints and Contexts* (kur. 45-54). Stanford: CSLI Publications.

Inkelas, S., & Downing, L. (2015). What is reduplication? Typology and analysis: Part 1/2 the typology of reduplication. *Language and Linguistics Compass, 9*(12), 491-528.

Katamba, F. (1978). How agglutinative is Bantu morphology? *Linguistics, 16*, 77-84.

Kenstowicz, M. (1994). *Phonology in Generative Grammar*. Cambridge, MA: Blackwell.

Kihore, Y., Massamba, D. P., & Msanjila, Y. P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1580

Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kosch, I. (2005). Discontinous elements in morphology. *South African Journal of African Languages, 3*, 161-172.

Leben, W. R. (1973). *Suprasegmental Phonology.* MIT: Tasnifu ya Uzamivu.

Massamba, D. P. (1982). *Aspects of Accent and Tone in Ci-Ruuri.* Inciana University: Tasnifu ya Uzamivu.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

McCarthy, J. J. (1981). A prosodic theory of nonconcatenative morphology. (3, Mhar.) *Linguistic Inquiry, 12*, 373-418.

McCarthy, J. J. (1982). Prosodic templates, morphemic templates, and morphemic tiers. Kwenye H. van der Hulst, & N. Smith (Wahar.), *The Structure of Phonological Representations* (kur. 191-223). Dordrecht: Foris Publication.

McCarthy, J. J., & Prince, A. S. (1990). Foot and word in prosodic morphology: The Arabic broken plural. *Natural Language & Linguistic Theory, 8*(2), 209-283.

McCarthy, J. J., & Prince, A. S. (1995). Prosodic morphology. Kwenye J. Goldman (Mhar.), *The Handbook of Phonological Theory* (kur. 318-366). Cambridge, Mass: Blackwell Publishers.

Mchombo, S. (2004). *The Syntax of Chichewa.* Cambridge: Cambridge University Press.

Myers, S. (1998). Aux in Bantu morphology and phonology. Kwenye L. Hyman, & C. Kisseberth (Wahar.), *Theoretical Aspects of Bantu Tone* (kur. 231-264). Stanford: Center for the Study of Language and Information.

Ngonyani, D. (2006). Attract F and verbal morphology in Kiswahili. *The Linguistic Review, 23*(1), 35-66.

Novotna, J. (2000). Reduplication in Swahili. *Swahili Forum, VII*, 57-73.

Park, J.-I. (1997). Disyllabic requirement in Swahili morphology. *U Penn Working Papers on Linguistics, 4*(2), 245-257.

Spencer, A. (1991). *Morphological Theory.* Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili.

Wiltshire, C., & Marantz, A. (2000). Reduplication. Kwenye G. E. Booij, C. Lehman, J. Mugdan, W. Kisselheim, & S. Skopeteas (Wahar.), *Morphologie 1. Halbband* (kur. 557-567). Berlin & New York: De Gruyter.

 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.